

Mpito: mwanzo mzuri wa shule

Miongozo ya kusaidia familia kukamilisha Taarifa ya Kujifunza na Maendeleo ya Mpito

Kwa nini mwanzo mzuri wa shule ni muhimu?

Mwanzo mzuri wa shule unaweza kumsaidia mtoto wako kujifunza vyema pamoja na kujisikia furaha anapohamia kutoka chekechea hadi shuleni na katika masomo yake ya baadaye.

Mabadiliko chanya pia husaidia mwendelezo wa masomo na ukuaji wa mtoto wako, kwa kuendeleza uzoefu wa awali na wa sasa wa mtoto wako ili kumsaidia kujisikia salama, kujiamini na kushikamana. Mwanzo mzuri wa shule unaweza pia kuwasaidia kustahilimia zaidi.

Taarifa ya Kujifunza na Maendeleo ya Mpito ni nini?

Huduma za watoto wachanga, shule, Utunzaji wa Nje ya Masaa ya Shule (OSHC) na familia hufanya kazi pamoja ili kusaidia ufunzaji pamoja na ustawi wa watoto. Wanashiriki habari kwa kutumia Taarifa ya Kujifunza na Maendeleo ya Mpito (TLDS). Hii imeandikwa na huduma ya utotoni kwa kila mtoto anapoenda shule.

TLDS hushiriki maelezo kuhusu kujifunza, kukua pamoja na ustawi wa mtoto wako kati ya huduma za utotoni na shule. TLDS hutoa mtazamo wa haraka wa maslahi, ujuzi na uwezo wa mtoto wako na kubainisha mbinu za mtu binafsi na mikakati ya kufundisha ili kumsaidia mtoto wako.

TLDS inaweza kukusaidia wewe kuelewa na kusaidia ujifunzaji wa mtoto wako anapoanza shule. Taarifa katika TLDS huwasaidia walimu wa Msingi (Foundation) kumfahamu mtoto wako na kupanga mipango ifaayo ya ufundishaji. Ikiwa mtoto wako atakuwa katika OSHC, TLDS husaidia kupanga wakati wake huko pia.

TLDS ina baadhi ya maelezo ya kibinafsi ikiwa ni pamoja na jina la mtoto wako, siku ya kuzaliwa na picha yake, pamoja na jina lako na maelezo ya mawasiliano. Inaweza pia kuwa na jina na maelezo ya mawasiliano ya wataalamu wengine wa utotoni ambao wamemsaidia mtoto wako.

Kuchangia katika TLDS ya mtoto wako ni mojawapo ya mpito kuelekea shughuli za shule wewe na mtoto wako mnawenza kushiriki pamoja kabla ya shule kuanza.

Je, ninavezaje kupata TLDS ya mtoto wangu?

Huduma ya utotoni ya mtoto wako itakupa kiungo cha zana ya Mtandaoni ya TLDS. TLDS Mkondoni ndiyo njia bora ya kukamilisha TLDS.

Ikiwa huwezi kutumia zana ya mtandaoni, unaweza kuomba nakala ya karatasi badala yake.

Je, ninajaza sehemu gani ya TLDS?

Sehemu ya 1 na 1.1 hujazwa na mwalimu wa utotoni wa mtoto wako.

Sehemu ya 1.2 inaweza kukamilishwa na mwalimu wa utotoni wa mtoto wako ikiwa mtoto wako ana ucheleweshaji wa ukuaji au ulemavu. Wataalamu wengine wanaomsaidia mtoto wako wanaweza pia kuongeza sehemu hii.

Sehemu ya 2: *Mtoto* inakamilishwa na mtoto wako na mtu mzima anayemfahamu vyema. Huyu anaweza kuwa wewe, au mwalimu wao wa utotoni.

Sehemu ya 3: *Familia* ni kwa ajili yako kujaza. Maoni yako ni muhimu. Sehemu hii ina maswali ya kukusaidia kushiriki mapendeleo ya mtoto wako, pamoja na mawazo na matumaini yako kwa mtoto wako shuleni. Kujibu maswali haya kunaweza kuwasaidia walimu na wafanyakazi wa OSCH (ikiwezekana) kujibu na kumwelewa mtoto wako, jambo ambalo litasaidia kujifunza na kukua kwake.

Nini kitokea baada ya TLDS kukamilika?

Baada ya kukamilisha TLDS, mwalimu wako wa utotoni atakupa nakala iliyokamilika.

Mwalimu wako wa utotoni pia atashiriki TLDS iliyokamilishwa na shule na huduma ya OSCH ya mtoto wako (ikiwa inatumika).

Ikiwa wewe huna uhakika mtoto wako atasomea shule ngani, mwalimu wako wa utotoni atakupa nakala ya pili ya TLDS. Wewe unaweza kutoa hii kwa shule unapomsajili mtoto wako.

Kama wewe hutajaza Sehemu ya 3: *Familia*, mwalimu wa utotoni wa mtoto wako bado atashiriki sehemu zingine zilizokamilishwa na shule na huduma ya OSCH (ikiwa inafaa) na kukupa nakala ya kile kinachoshirikiwa.

Utafiti pamoja na maoni kutoka kwa shule yameonyesha kuwa kushiriki maelezo haya kunasaidia mabadiliko ya shule kwa mafanikio. Ikiwa wewe ungependa kutoshiriki TLDS na shule ya mtoto wako, tafadhalii jadili hili na mwalimu wa utoto wa mtoto wako.

Taarifa iliyo sahihi na salama husaidia wataalamu wa elimu pamoja na wataalamu wa utunzaji kutoka Victoria kuwa na ujuzi pamoja na taarifa zinazohitajika ili kuhakikisha ustawi na usalama wa mtoto.

Kwa habari zaidi tembelea, <https://www.vic.gov.au/information-sharing-schemes-and-the-maram-framework>.

Kwa habari zaidi

Ili kujifunza zaidi, wewe unaweza kutembelea www.vic.gov.au/transition-school-resources-families

Taarifa hii pia inapatikana katika idadi ya lugha za jumuiya kwenye kiungo kinachofana:
www.vic.gov.au/transition-school-resources-families